Nassir ahimiza umoja na upendo

Mheshimiwa Shariff Nassir ...aonekana katika hafla hiyo.

WALIMU WA Madrasa za Kiisilamu wanahitaji kusaidiwa sana na kutukuzwa pia kwani wao wanafanya kazi muhimu sana ya kueneza dini ya Mwenyezi Mungu. Hayo yalisemwa na mwenyekiti wa Tawi la Mombasa la Kanu ambaye pia ni Waziri mdogo wa Biashara, Mheshimiwa Shariff Nassir, katika ukumbi wa Sakina siku ya Jumapili tarehe 14 Septemba mwaka huu mnamo saa tatu asubuhi, alipokuwa akiwahutubia walimu wa Madrasa za Kiislamu kutoka Madrasa zote za Mombasa, pia zikiwamo Madrasa kutoka Kisauni, Likoni na Changamwe.

Nassir, akiwa mpole namchangamfu, alihakikishia walimu hao kwamba ilikuwa ni furaha kubwa kwake kukutana nao ili ajue matatizo yao.

Sharifu aliwasifu mno walimu hao na kuwapongeza kwa vile kufanya kazi zao bila ya kubugudhiana na kutoana makosa ya kuvunjana moyo ambayo huleta chuki na hasama kati ya waalimu ambao kazi yao ni ile ile moja ya kueneza dini ya Mungu.

Akiendelea, alisema kwamba Madrassa zote zinaweza kusaidiwa kwa njia ya Harambee.

Waziri, huku akishangiriwa kwa Takbira aliwataka walimu wa Madrasa zote wachague siku moja wajumuishe wanafunzi wao wote, waimbe Kasida na kwaya za Kiisilamu ili wapate kuchagua Madrasa zilizo mbele zaidi, ili zile zilizo nyuma zipate kujifunza kwa wengine, naye angekuwa tayari kujumuika na Madrassa hizo mchana kutwa na pia angeghariimia chakula kwa Madrasa zote zitakazoalikwa.

Shariff, alikubali ombi la walimu la kuongoza Harambee ya kujengwa "Quran House" ambayo ingesaidia kulipia mishahara ya walimu na pia kutoa nafasi za malazi kwa walimu wanaokosa maskani. Mgeni Mashuhuri katika Harambee hiyo, Waziri alisema kwamba, atakuwa Rais wetu mpendwa wa Kenya Bw. Moi.

Mhe. Nassir pia aliwaalika walimu hao katika hafla ya kufungua Madrasa-l-Hudaa hapo Guraya tarehe 26 mwezi wa Oktoba mwaka huu.

Aliwataka wafike kwa wingi na wanafunzi wao ili waoneshe umoja wao katika kufungua Madrasa ya mwanzo kujengwa kwa Harambee.

Mhe. Nassir alimaliza hotuba yake kwa kuita mwito wa Waisilmau kurehemeana popote pale walipo na kusema kwamba mwanadamu siku zote na ajitolee kwa nja ya Mungu ili apate shufaa baade ya kufa kwake. Alikariri kwamba yeye ni mtu wa Mungu kwa hivyo hajali kutoa msaada hata mkubwa kiasi gani kwa ajili ya dini ya Mungu.

Alisema, akifanya hivyo ndipo anapo barikiwa. Aliongeza kwamba yeye hakubaliani na tabia ya kuwaingiza walimu wa dini katika siasa, kwani kiongozi mara tu akianza kufanya hivyo, huwa ameanza kuleta machafuko kwa walimu hao.

Mwisho, Nassir aliwapa walimu hao shillingi mia moja kila mmoja wao, zikiwa kama kahawa yao.

Pia katika hafla hiyo, alihutubia Maalim Kassim Mwinyi wa Madrassa Annajaa ambaye pia alikuwa ndiye mwenyekiti wa mkutano huo.

Maalim Kassim, alimuahidi Sharif kwamba siku zote walimu wa dini ya Kiisilamu wako bega kwa bega naye nawakati wowote atakapowahitaja wataitikia mwito wake bila ya kuchelewa.

Kassim, alimuomba Nassir azidi kuwangalia walimu kwa njia za misaada kwani wao wana kazi muhimu katika taifa hili nayo ni kuwafundisha wanafunzi dini yao ili wazidi kuwa viongozi wazuri hapo mbeleni.

Vile vile aliwaomba walimu wafike hapo hapo ukumbi wa Sakina jumapili ya tarehe 21 mwezi huu ili waunde chama kipya cha walimu wa Madrassa na pia wachague viongozi wapya wa chama hicho. Mkutano ulifungwa kwa kumuombea malazi mema Marehemu babake Shariff Nassir na Waisilamu wote kwa jumla.

TAIFA LA Oman kati ya mataifa ya Kiarabu limepata sifa kwa maongozi ya busara ya kiongozi wa nchi hiyo H. M. Sultan Qaboos bin Said al Said ambaye kila mara Mawaziri wake wapo chonjo kujadili shughuli na mipango inayokabili mataifa yote ya Kiarabu, na ulimwengu. Hapa Waziri wa Mashauri ya nchini Oman Seyyid Bader bin Soud bin Harib al Busaidy (watatu kutoka kushoto) anakutana na Waziri wa Mashauri ya nchini wa Saudi Arabia (wapili kushoto) wakati akiwasili nchini Saudi Arabia kwa mashauri muhimu kati Mawaziri wote wa Mashauri ya nchini katika mataifa ya Kiarabu. Waziri Seyyid Bader aliandamana na wakuu wa idhaa na Idara ya Habari kutoka Oman.

Mataifa ya Kiisilamu yaunga Jihad

...KUTANO wa kwanza wa ...hughuli za utangazaji wa ...isilamu katika ulimwengu ...ili ya mataifa ya Kiisilamu ...amerika nchini Indonesia na ...ipitsha azimio la kuunga ...mono msimamo wa Prince ...ahad wa Saudi Arabia ...ilyependekeza mapambano ya ...ihad kuwa ndio suluhisho la ...ake katika kutatua mzozo ...ilizushwa na Israel huko ...ashariki yakati na kupinga ...uazimio yote ya Umoja wa ...ataifa.

Akitangaza haya Muakilishi ...a Kenya katika Mkutano huo ...heikh Ahmed Mohamed ...hallam alisema "Mkutano ...uo ulipendekeza kuundwa ...wa Shirika la Habari la ...ataifa ya Kiisilamu na kuwa ...o makao yake mjini Mecca ...uko Saudi Arabia na kwamba ...ataifa yasiokuwa ya ...isilamu yafahamishwe vile ...aweli ulivyo kuhusu maoni ya ...aisilamu, na vile kutoa ...endekezo la kuundwa kwa ...utawi ya Shirika hilo kote ...limwenguni".

Lengo hili pia lilipendekeza ...uundwa kwa Shirika hilo ...mbalo litasimamiwa na Umoja ...a Waisilamu katika ...limwengu (World Muslim ...eague) yaani Rabita.

Mkutano huo alifahamisha ...heikh Msallam pia uli-...endekeza kuundwa kwa Chuo ...ha Kuwafunza Waandishi wa ...isilamu na mji wa Beirut ...upendekezwa kuwa makao ya ...huo hicho.

Sheikh Msallam alisema ...Kanu Mjumbe wa Kenya ...liweza kuufahamisha ...limwengu vile Maongozi ya ...yayo ya Mtukufu Rais Moi na ...eikali yake yanavyofaulu ...uwatumikia wananchi wote ...a Kenya bila ubaguzi wa dini, ...ila kabila au rangi ya mtu ...wake". Alisema "Kama ...humbe wa Kenya niliweza ...imarisha sifa ya uhuru wa ...taifa hili nchini Kenya na vile ...eikali inavyotoa uhuru huo ...alingana na katiba ya taifa".

Alisema "Umma wa ...isilamu kutoka mataifa yote ...ilurahia msimamo huo wa ...enya na hasa kuona kwamba ...aisilamu wanashirikiana ...kamilifu na ndugu zao wa ...enya katika mipango yote ya ...ymishi na ujenzi wa taifa ...ao".

Sheikh Msallam alisema "...iata za Mtukufu Rais Moi ...atika mataifa ya Kiarabu ...ewezi kuufahamisha ...limwengu vile Kenya inavyo-...ndelea na msimamo wa Kenya ...atika mambo yote yanayo-...ahidi ulimwengu".

...heikh Ahmed Mohamed Msallam

DARAJA LA ZAMANI LA NYALI

HAITAKUWA JAMBO la busara kwa serikali yetu kushirikiana na azimio la kuangamiza daraja la zamani la Nyali kwa sababu ya kujengwa daraja jipya. Kipya kinyemi Waswahili wasema, na kwamba kile cha zamani ni lazima kutuzwa ili kuhifadhika na kuendelea kutumikia taifa. Historia za madaraja ni kubwa kama ulimwengu ulivyo... lakini ni mwenendo wa mataifa mengi kuhifadhi madaraja yao ya zamani na kuyawezesha kutoa utumishi unaofaa ingawa daraja mpya zinapatikana.

Tunatoa mwito kwa Waziri wa Mawasiliano Bw. Kosgey kufikiria kwa makini hatua ya kulikinga daraja la zamani la Nyali kwani daraja hilo linaendelea kutoa utumishi. Ni daraja lililokatika sehemu fupi kati ya Mombasa kisiwani na Bara ya Kaskazini kutoka makao makuu. Na ni daraja inayokaribiana sana na mahoteli yote ya Utalii kaskazini ya kisiwa cha Mombasa.

Daraja la zamani la Nyali ni pambo la kiutalii Mombasa, ni kiungo muhimu kinachozidi kutoa utumishi unaofaa, na bila ya shaka lingali na umri wa kutoa utumishi. Haitakuwa jambo la busara kulivunja daraja hilo. Viongozi kama wametoa mwito kwa Waziri wa Mawasiliano nchini Kenya Bw. Kosgey kufikiria swala hili kwa makini. Kuangamiza si maongozi yanayotendeka Kenya.

Idara ya Maji Pwani imekuwa ikileta masumbuko makubwa kwa wananchi wa Mombasa wakati maji yakikatwa bila sababu. Tungetoa mwito kwa Mkuu wa Idara ya Maji Bw. Chege kukutana na maafisa wake na kujadili swala hili. Tumepata ushahidi wa kutosha kwa raia. Injinia Mkuu wa Maji Pwani Bw. Dugdale ametoa mwito kwa wananchi kufika katika afisi yake ili kumuhakikishia tatizo hili. Haitakuwa halali kamwe baadhi ya mafundi wa mitereji kufika katika nyumba za watii wa sheria na kuwa wajeuri na bila ya kuhakikisha kama maji yamelipwa au la watu hukata maji na kutatiza jamii. Maongozi ya Kimabavu si kwa Kenya kwani Mombasa nayo ni sehemu ya Kenya na ni lazima wananchi kutendewa na kutumikiwa vile inavyofaa bila ya kuwasumbua. Wahalifu wa sheria za maji ni lazima kutambuliwa kwanza kabla ya maji kukatwa na kuleta tatizo lisilo msingi.

NINI UBAYA WA MADRASAZA QURANI?

PONGEZI kwa Raisi wetu kwa kutoa uhuru wa kuabudu katika nchi ya Kenya. Fursa hii, inatumiwa na dini mbali mbali kwa kuwawashia mwangaza wa dini watoto wao ili mbele yao kusiwe na kiza, yaani, wanafunzi wamjue Mola, Mtume wao, wajue amri na makatazo ya dini yao.

Wanafunzi wakiyaelewa hayo, watamcha Mola wao, watafata Mtume wao na wataitii serikali yao kwani kutii serikali pamoja na kiongozi wake ni moja ya mafunzo ya Dini ya Kiisilamu. Kila Mwisilamu alijua jambo hili.

Mafunzo yote ya dini ya Kiisilamu, yamo katika Qurani tukufu na Khadithi za Mtume. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba mtoto asiyesomeshwa Qurani, hana msingi wa dini yake na mwisho wake lazima atakuwa mpotofu.

Ajabu ni kwamba, katika nchi hii hii ambayo ina uhuru wa kuabudu, kuna baadhi ya Wasilamu ambao wanasimama kidete kuipinga Qurani isisomeshwe katika Madrassa au maskuli mpaka pale mtoto amalizapo masomo ya Kiskuli. Twauliza, jee tusubiri mtoto amalize shule ya msingi au ya upili au kidato cha sita au Chuo Kikuu ndipo mtoto aanze kufundishwa Qurani?

Kumbukeni methali: Lidongo upatize ulimaji. Mtoto barobaro atakubali wapi kukaa chini akaanza Alifu kwa kijiti cha makuti? Tunao ushahidi katika magazeti ya hapa hapa nchini watu (wengine wao wakiwa Waisilamu) ambao wamepitisha katika mikutano yao kwamba mtoto kumsomesha Qurani, ati ni kumrudisha nyuma. Suali Jee kumpeleka mbele ni kumsomesha nini? Angalia Taifa Leo la tarehe 14.1.80 na pia Taifa Leo la tarehe 24.9.79 na kadhalika katika Daily Nation la tarehe 4.7.79.

Humo utakuta maneno ya kuvunja nguvu usomeshaji wa Qurani. Japo kwamba habari hizi zimekuwa kuu kuu lakini wachaji Mungu wa kikweli kweli, wanayaona maneno haya ni fitna ki bwa sana kwa Waisilamu. Na yataka ndugu zanguni tuilinde dini yetu, kwani Muisilamu akikosa kujua Qurani huwa ameangamia.

Ikiwa leo kuna watu ambao wanaona kuwa kumsomesha mtoto Qurani ni kumpotezea wakati, kesho watu hawa watasema mengi zaidi na mabaya zaidi. Na iwapo Waisilamu watakaa kimya ndipo watakapo twaa uwanja wa kueneza kasumba zao. Lakini mimi kama mzazi mtoto wangu, kwanza atasoma Qurani, hata ikiwa ni chini ya mnazi.

Said Burhan,
MOMBASA.

SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku la Posta 87270, Mombasa KENYA

Coastweek

SWAHILI CROSSWORD NO. 96



KWENDA KULIA:

1. Ulichokitupa pwani kingojee .....
4. Ama
6. Peleka mtu mahali
8. Uji wa mwana mchanga
9. Ondoa nguo juani
11. Kitongoji karibu ya Malindi Kenya
12. Kula kwa ndimi
14. Kinyume cha hana
16. Kongwe, ya kale
17. Awashike
20. Mahali

KWENDA CHINI:

1. Umaskini
2. Ufuo, kandokando ya bahari
3. Ichukue
4. Si p.m.
5. Toana roho
7. Namna ya kuandaa
10. Uwe kila mal..ali
11. La samaki
13. Miti ya sukari
15. Kinyume cha EA
17. Kama No. 4 kwenda chini
18. AK haibadiliki
19. Nusu ya neno wote

JINA .....

SANDUKI LA POSTA .....

KWENDA CHINI:

2. ENGA, 3. DARAJA, 4. UTANDU, 6. OTA, 8. BINDA, 10. DOMO, 11. BONDE, 14. EMBE, 18. LA, 19. OA.

JEMBE

UNGA SAFI NO. 1

WA MAHINDI

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 94:

[1] Mr Said Hussein, Sanduku la Posta 46, Kwale,

[2] Mr M. Kumenjwa, Sanduku la Posta 90440, Mombasa,

[3] Mr M. S. Kussema, Sanduku la Posta 80149, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 94 —

KWENDA KULIA:

1. TENDEGU, 5. TAO, 7. NGARIBA, 9. INDA, 12. JANDO, 13. ONEA, 15. DUMA, 16. UA, 17. DUBU, 20. NGAMA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muharir, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 2.10.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.